

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MABADILIKO YA WAJUMBE WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**

Spika wa Bunge Mhe. Job Ndugai (Mb) amefanya mabadiliko ya Wajumbe wote Ishirini na nne (24) wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kuunda upya kamati hiyo na kuteua wajumbe Wapya Kumi na sita (16) ambao pia watakuwa ni wajumbe katika kamati nyingine za Kudumu za Bunge.

Mabadiliko haya yamelenga kuwawezesha Wabunge kujifunza na kujipatia uelewa na uzoefu zaidi katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Kamati za Bunge ambapo Wabunge wote waliokuwa Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI hapo awali, wamepangiwa Kamati zingine kwa nia ya kuboresha Utekelezaji wa majukumu ya kibunge.

Msingi wa Mabadiliko haya unatokana na Ibara ya 96 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayolipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mamlaka ya kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri linavyoona inafaa kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake na Kanuni ya 116 (3) – (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inampa Spika Mamlaka ya kuteua Wabunge ili wawe Wajumbe katika Kamati mbalimbali za Bunge ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya kuongeza, kubadilisha au hata kupunguza idadi ya Wajumbe katika Kamati za Kudumu za Bunge.

Kwa mujibu wa waraka Na.5/2016 wa Mhe. Spika kwa Wabunge wote wa Tarehe 7 Oktoba, 2016, Mabadiliko haya yataanza kutekelezwa mara moja kuanzia mwezi huu Oktoba, 2016 ambapo Wajumbe husika watakutana kwa ajili ya kufanya Uchaguzi wa Viongozi wao na kuandaa Ajenda za Vikao vya Kamati. Orodha ya wajumbe wapya 16 wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI na orodha ya wajumbe 24 waliobadilishwa kutoka kamati hiyo na Kamati mpya walizohamishiwa imeambatishwa.

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano
Ofisi ya Bunge
DODOMA

9 Oktoba, 2016.

ORODHA YA WAJUMBE WAPYA WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI

NA.	JINA	KAMATI YAKE NYINGINE
1.	Mhe. Asha Abdullah Juma, MB	Pia ni Mjumbe wa Katiba na Sheria
2.	Mhe. Daniel Edward Mtuka, MB	Pia ni Mjumbe wa Sheria Ndogo
3.	Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, MB	Pia ni Mjumbe wa Huduma na Maendeleo ya Jamii
4.	Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, MB	Pia ni Mjumbe wa PAC
5.	Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, MB	Pia ni Mjumbe wa Huduma na Maendeleo ya Jamii
6.	Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, MB	Pia ni Mjumbe wa Katiba na Sheria
7.	Mhe. Joseph Kizito Mhagama, MB	Pia ni Mjumbe wa Katiba na Sheria
8.	Mhe. Juliana Daniel Shonza, MB	Pia ni Mjumbe wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama
9.	Mhe. Kemirembe Julius Lwota, MB	Pia ni Mjumbe wa Ardhi, Maliasili na Utalii
10.	Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, MB	Pia ni Mjumbe wa Huduma na Maendeleo ya Jamii
11.	Mhe. Mary Deo Muro, MB	Pia ni Mjumbe wa Miundombinu
12.	Mhe. Martha Mlata, MB	Pia ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira
13.	Mhe. Masoud Abdalla Salim, MB	Pia ni Mjumbe wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama
14.	Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, MB	Pia ni Mjumbe wa Nishati na Madini
15.	Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, MB	Pia ni Mjumbe wa Viwanda , Biashara na Mazingira
16.	Mhe. Yussuf Kaiza Makame, MB	Pia ni Mjumbe wa Nishati na Madini

ORODHA YA WALIOKUWA WAJUMBE WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI NA KAMATI WALIZOHAMISHIWA

NAMBA	JINA	KAMATI ALIYOHAMISHIWA
1.	Mhe.Hassna Sudi Katunda Mwilima,Mb	Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama
2.	Mhe.Constantine John Kanyasu,Mb	Uwekezaji wa Mitaji ya Umma(PIC)
3.	Mhe. Muhammed Amour Muhammed,Mb	Uwekezaji wa Mitaji ya Umma(PIC)
4.	Mhe. Sixtus Raphael Mapunda,Mb	Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC)
5.	Mhe.Juma Kombo Hamad,Mb	Katiba na Sheria
6.	Mhe. Mattar Ali Salum,Mb	Kilimo, Mifugo na Maji
7.	Mhe.Savelina Sylvanus Mwijage,Mb	Huduma na Maendeleo ya Jamii
8.	Mhe. Khalifa Mohammed Issa,Mb	Utawala na Serikali za Mitaa
9.	Mhe.Abdallah Haji Ali,Mb	Hesabu za Serikali(PAC)
10.	Mhe. Waitara Mwita Mwikabe,Mb	Utawala na Seikali za Mitaa
11.	Mhe. Khamis Yahya Machano,Mb	Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama
12.	Mhe.Sikudhani Yasini Chikambo,Mb	Huduma na Maendeleo ya Jamii
13.	Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka,Mb	Miundombinu
14.	Mhe. Mgeni Jadi Kadika,Mb	Hesabu za Serikali za Mitaa(LAAC)
15.	Mhe. Hussein Nassor Amar,Mb	Huduma na Maendeleo ya Jamii
16.	Mhe.Richard Philip Mbogo,Mb	Hesabu za Serikali za Mitaa(LAAC)
17.	Mhe. Grace Victor Tendega,Mb	Huduma na Maendeleo ya Jamii
18.	Mhe. Elibariki Emmanuel kingu,Mb	Sheria Ndogo
19.	Mhe. John Peter Kadutu,Mb	Hesabu za Serikali za Mitaa(LAAC)
20.	Mhe.Azza Hamad Hillal,Mb	Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)
21.	Mhe. Zaynab Matitu vulu,Mb	Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC)
22.	Mhe.John Wegese Heche,Mb	Nishati na Madini
23.	Mhe.Vuma Hole Augustine,Mb	Uwekezaji wa Mitaji ya Umma(PIC)
24.	Mhe.Yahya Omari Masare	Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama